



TAARIFA KWA UMMA

Mnamo tarehe 24 Julai 2014 Benki Kuu ya Tanzania iliweka chini ya usimamizi maalumu (statutory management) benki ya FBME Bank Limited (FBME). Hatua hii ya Benki Kuu ilitokana na Notisi iliyotolewa tarehe 15 Julai 2014 na Taasisi ya Marekani inayopambana na Uhalifu wa Kifedha “the US Financial Crimes Enforcement Network” kwa kifupi FinCEN, iliyoituhumu FBME kuwa ni taasisi inayojihusisha na biashara ya utakatishaji wa fedha haramu (money laundering) na hatua ya Benki Kuu ya Cyprus kuliweka tawi la FBME lililopo nchini Cyprus chini ya uangalizi maalumu (special administration). Katika Notisi hiyo, FinCEN ilitoa kusudio la kuifungia FBME kutotumia mfumo wa kibenki wa Marekani (US financial system).

Tarehe 29 Julai, 2015, FinCEN ilitoa uamuzi wa kuifungia FBME kutumia mfumo wa kibenki wa Marekani. FBME walifungua kesi katika Mahakama huko Marekani (US District Court for the District of Columbia) wakiiomba mahakama kutengua uamuzi wa FinCEN. Hatimaye siku ya tarehe 14 Aprili, 2017 mahakama ilitoa uamuzi ambao unairuhusu FinCEN kuendelea na utekelezaji wa uamuzi wake wa mwisho (Final Rule) ambao unaifungia benki ya FBME kutumia mfumo wa kibenki wa Marekani.

Uamuzi huo wa mahakama unaongeza athari kwa kiwango kikubwa katika uendeshaji wa FBME kwa kuwa haitaweza tena kufanya miamala ya kibenki ya kimataifa na kupata huduma za mfumo wa kibenki na hivyo itashindwa kutoa huduma muhimu kwa wateja wake kwa mujibu wa leseni waliyopewa.

Kwa kuzingatia athari zinazotokana na uamuzi wa mwisho wa FinCEN, kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 58(2)a, 11(3)(i), 61(1) na 41(a) vya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 (the Banking and Financial Institutions Act, 2006), Benki Kuu ya Tanzania imesimamisha shughuli zote za FBME Bank Limited; kufuta leseni yake ya kufanya shughuli za kibenki; kuiweka chini ya ufilisi; na kuiteua Bodi ya Bima ya Amana (DIB) kama mfilisi kuanzia tarehe 8 Mwezi Mei, 2017

**BENKI KUU YA TANZANIA
5 MEI 2017**